

## **Shule ya chekechea wazi - Åpen barnehage**

**Shule ya chekechea wazi** ni mahali pa kukutana wakati wa mchana kwa familia zilizo na watoto wenye umri wa miaka 0-6. Si lazima kutuma ombi la kupata nafasi ili uweze kushiriki. Katika chekechea wazi, mtoto wako anapata uzoefu na mwillingiano wa kijamii na kucheza kabla ya kuanza katika shule ya chekechea ya kawaida.

Katika Bergen kuna shule za chekechea wazi 15 za kibinasi katika sehemu tofauti kadhaa za manispaa.

### **Ni nini hufanyika katika chekechea wazi?**

- Shule ya chekechea iliyo wazi ni shughuli ya kielimu inayoongozwa na mwalimu wa chekechea.
- Unaweza kuja wakati wowote unapotaka wakati wa masaa ya ufunguzi wa chekechea.
- Kushiriki katika shule za chekechea wazi ni bila malipo. Katika baadhi ya chekechea wazi unapaswa kulipa kiasi kidogo kwa ajili ya shughuli, chakula na vifaa (kutoka krona tano kwenda juu ).
- Una wajibu wa kumchunga mtoto wako kwa michezo, shughuli na kuchangia kwa usafi na kuweka utaratibu.
- Mifano ya shughuli: mikutano ya pamoja , nyimbo na muziki, fasihi na matukio, sanaa na shughuli za ubunifu, shughuli za kimwili na kutembea, kupika na milo.
- Mtoto wako anaweza kucheza na watoto wengine na kukuza lugha, ustadi wa kimwili na kijamii.
- Utaweza kujuana na familia zingine.
- Unaweza kupata taarifa, ushauri na mwongozo kuhusu ustawii na maendeleo ya watoto, chekechea na jinsi ya kutuma maombi ya kupata nafasi ya shule ya chekechea na huduma zingine kwa familia zenye watoto wadogo.

